



Tarehe 2 Februari 2011

VICHANGA VILIVYOTUPWA JALALANI MWANANYAMALA KWA KOPA

Sikika imepokea kwa masikitiko makubwa sana habari za kugundulika kwa miili 10 ya watoto wachanga waliokuwa wametupwa katika shimo dogo la takataka huko karibu na eneo la makaburi ya Mwananyamala kwa Kopa tarehe 31 Januari 2011. Kwanza tunatanguliza pole kwa wahusika pamoja na wakazi wa eneo ambalo vichanga hivi vilitupwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kwa vyombo vya habari, wazazi wa baadhi ya vichanga hivyo wanajulikana na wanafuatiliwa. Taarifa hiyo pia inadai kwamba kuna uwezekano kuwa wahudumu wa chumba cha kuhifadhi maiti cha Mwananyamala wanaweza kuwa wamehusika kwa namna moja au nyingine katika kadhia hii ya uzembe.

Pia, taarifa hiyo ilidai kwamba baadhi ya vichanga hivyo vilivyotupwa jalalani vilikuwa ni mimba zilizoharibika, wakati vitatu vilikutwa na utambulisho unaoihusisha hospitali ya Mwananyamala. Vichanga vyote kumi vilikutwa vimeviringishwa shuka la Hospitali ya Mwananyamala.

Sikika inaona uwezekano wa hospitali ya Mwananyamala kuhusika na tukio hili kwa sababu zifuatazo. Kwanza, kumbukumbu za vichanga vitatu zinaihusisha hospitali hii moja kwa moja. Pili vichanga vyote vilikuwa vimeviringishiwa shuka la hospitali hiyo. Tatu, hospitali hiyo imeshakiri kwamba baadhi ya wafanyakazi wake wanaweza kuwa wamehusika, hasa wa chumba cha kuhifadhi maiti.

Hoja kwamba baadhi ya vichanga vilikuwa ni mimba zilizoharibika haitoi utetezi wa vichanga hivyo kutupwa kwenye jalala la mwananchi wa kawaida. Kwamba hospitali hii haikutekeleza wajibu wake wa kuharibu miili hiyo katika maeneo ya hospitali kwa kutumia vifaa na taratibu zilizokubalika kitaalamu.

Katika taarifa ya habari ya TBC1 jana saa mbili usiku, kuna wananchi walitoa ushuhuda kwamba waliombwa na nesi wa hospitali ya Mananyamala mwili wa maiti ya mtoto wao aliyekuwa amefia tumboni. Taarifa hii inapingana na taarifa ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kwamba kuna wananchi wanaoomba kuzikiwa vichanga vyao kutokana na sababu za umasikini.

Ni kutokana na sababu hizi hapa juu Sikika inahisi kwamba hospitali ya Mwananyamala na Manispaa ya Kinondoni kwa pamoja wanatakiwa wachunguzwe. Ni kwa mantiki hii Sikika inaamini kwamba Tume iliyoundwa na Manispaa ya Kinondoni kuchunguza kadhia hii haina uhalalali wa kufanya kazi hiyo. Hii ni kutokana na kwamba tume hiyo imeundwa na mhusika anayetakiwa kuchunguzwa na kwamba wajumbe wa tume ni wahusika wa kadhia hii.

Uzoefu wa Sikika kwenye matukio mbalimbali ya uzembe, ukiukaji wa taaluma, na kutokuwajibika kwa watendaji wa hospitali ya Mwananyamala tangu 2007 unaonyesha kuwa tume zinazoundwa huishia kulinda wahusika. Hivyo basi Sikika inashauri yafuatayo:

- Kuundwa kwa Tume huru isiyohusisha wafanyakazi wa Manispaa ya Kinondoni wala Hospitali ya Mwananyamala
- Jeshi la polisi lifanye kazi yake ya kipelelezi na kufikisha watuhumiwa mikononi mwa vyombo vya sheria badala ya kuwa miongoni mwa wajumbe wa tume iliyoundwa.
- Wahusika wa vichanga vilivyotupwa wajitokeze na kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi na Tume huru itakayoundwa.
- Kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu watendaji wote watakaobainika kuhusika na kadhia hii
- Tume hiyo itakayoundwa ichunguze pia madai ya wananchi ya kuombwa na manesi maiti za vichanga vyao.

Mr. Irenei Kiria

Executive Director of Sikika, P.O.Box 12183 Dar es Salaam,
Tel: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, Email: info@sikika.or.tz, Website: www.sikika.or.tz